HOTUBA YA MGENI RASMI, MHE. JABIR M. SHEKIMWERI

(MKUU WA WILAYA YA MPWAPWA)

KATIKA MKUTANO WA ALAT MKOA WA DODOMA, TAREHE 28.08.2016

Mhe, Mwenyekiti wa ALAT MKOA, (White Zuberi-Mkt Kongwa Dc)

Kaimu Katibu wa ALAT MKOA, (Mkurugenzi Mtendaji-Mpwapwa)

Mstahiki Mega Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma, (Jaffer Mwamwenda)

Waheshimiwa Wabunge,

Katibu Tawala Msaidizi Menejimenti Serikali za Mitaa, (Ndugu Emmanuel Kuboja)

Wenyeviti wa Halmashauri,

Wahe. Madiwani,

Wakurugenzi Watendaji,

Sekretarieti ya ALAT (M),

Wageni waalikwa,

Wanahabari,

Mabibi na Mabwana!

Asalaam aleykum, ninawasalimu nyote katika jina la Bwana.

Awali ya yote sina budi kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutupa uzima huu tulio nao.lakini pia nawashukuru nyote kwa kuchagua Mpwapwa kufanyia mkutano na kunialika kuwa mgeni rasmi.

Mhe mwenyekiti,

Napenda kuchukua nafasi hii karibisheni sana katika wilaya yetu ya Mpwapwa. Wilaya yetu ipo shwari na kuna ukalimu mkubwa. Kwa namna ya pekee nawashukuru ninyi nyote kwa kuhudhuria mkutano huu wa ALAT Mkoa unaounganisha Halmashauri zote za wilaya, Miji na Manispaa katika mkoa wetu wa Dodoma.

Lakini nitumie fursa hii kuwa pongeza wajumbe kuchaguliwa kwenye uchaguzi mkuu 2015 na kuziwakilisha Halmashauri zenu kwenye ALAT naamini kuwa mtaenda kutumia fursa hii kujenga timu imara ambayo kwayo imekuwa nguzo muhimu katika kushughulikia mikakati mbali mbali ya kuhakikisha kuwa wananchi wetu wanapata maendeleo endelevu . Ushirikiano huu uendelee na udumishwe daima. ***ALAT Oyeee!***

Ndugu Wajumbe,

Kupitia ALAT umejengeka utamaduni mzuri wa kufanya mikutano hii baada ya kutembelea miradi na kushirikisha changamoto mbali mbali kama;- ushiriki hafifu wa maandalizi, usimamizi hafifu wa wataalamu, uwajibikaji hafifu, uwepo wa ubadhirifu na ushirikishwaji mdogo wa jamii. Hivyo kuchelewa kukamilika kwa miradi, kuchelewa huduma kusudiwa, na wananchi kuichukia serikali. Kwa namna ya pekee kabisa ninawashukuru Wakurugenzi watendaji kwa uteuzi uliofanywa na Raisi kwa Wakurugenzi (2016), pamoja na timu zao za wataalamu kwa kazi nzuri ambayo mmekuwa mkiifanya kwa kushirikiana katika kutekeleza maazimio mbali mbali ambayo yamepitishwa kwa ajili ya ujenzi wa ustawi wa jamii yetu na taifa kwa ujumla. Pongezi hizi za dhati ziwaendee pia viongozi wa kisiasa kwa kusimamia Halmashauri zetu. Mmekuwa mkifanya kazi bega kwa bega, usiku na mchana, na kwa uzalendo mkubwa katika kuhakikisha kuwa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi inatekelezwa na kuhakikisha kuwa wananchi wetu wanapata huduma bora.

Rai yangu ili kuendana na dhima ya utendaji wa serikali ya awamu ya tano, ni vema sasa kuwe na vigezo sawia vya upimaji wa utekelezaji wa miradi inayorandana na kujiwekea utaratibu wa utoaji taarifa wenye kuzingatia matokeo (result based reporting system) mrejesho wa

Mhe mwenyekiti,

Katika utendaji wetu kazi hasa katika kusimamia na kutekeleza miradi ya maendeleo katika Halmashauri zetu, kumekuwa na changamoto mbali mbali kama vile miradi ya maendeleo kutekelezwa chini ya kiwango, wakandarasi kucheleweshewa malipo, Bajeti kutopata fedha zote hata hizo kidogo zinakuja kwa kuchelewa, nguvu za wananchi kutoungwa mkono na hivyo kuongeza miradi viporo na uanzishwaji holela wa miradi. Nachukua fursa hii kutoa rai kuwa tukiwa viongozi wa umma, tujikite katika kutatua changamoto hizo kwa kuchukua hatua mbali mbali na kusimamia kikamilifu utekelezaji wa miradi hiyo. Aidha serikali ya awamu ya tano, itarudi kuchukua hatua.

ALAT Oyeee! !!!!!,

Vile vile katika mkoa wetu kutakuwa na zoezi la kukimbiza mwenge kuanzia mwezi wa tisa, hivyo basi nitoe rai kwa viongozi wenzangu kuhakikisha kuwa mwenge unatendewa haki kwa kufanya maandalizi ya kutosha na stahiki kwa kuwa Mwenge wetu wa uhuru una manufaa makubwa hususani katika kuchochea maendeleo na ni kipimo tosha cha uzalendo wetu.mwaka uliopita mkoa ulifanya vizuri ulikuwa wa 11 ambapo wilaya ya Bahi ilikuwa ya 2 Kitaifa na ya 1 katika Mkoa.

Mhe mwenyekiti na ndugu wajumbe,

Hivi karibuni serikali imepitisha azimio za kuhamishia makao makuu ya kiutawala katika mkoa wetu. Jambo hili siyo tu jema ila ni neema na fursa kwetu tulio wenyeji. Tutumie fursa hii muhimu katika kuweka mipango mbali mbali thabiti ya kimaendeleo. Hivyo basi Kila Halmashauri iweke mipango ya kuibua fursa mbali

mbali za uwekezaji na kuandaa mazingira rafiki ya uwekezaji. Halmashauri zijikite katika kupima maeneo mbali mbali, kuainisha vivutio vya uwekezaji na kuvitangaza. Ni vema pia kutenga maeneo ya wajasiria mali, kudumisha ukarimu, na usafi kwa ujumla.

Ndugu zanguni, na wanasiasa wenzangu, wahenga walinena kuwa “mbio za sakafuni huishia ukingoni”, “tena kakuna marefu yasiyokuwa na ncha”. Hata kama mioyo yetu ina dhamira ya dhati yakuendelea kuwatumikia wananchi, pasipo kubadilika hakutakuwa na mafanikio. Wakati wa mabadiliko ni sasa muhimize wananchi kufanya kazi na tutende kazi kwa weledi kwa kuzingatia Sheria, Taratibu na Kanuni. Watendaji acheni utendaji wa mazoea na wanasiasa epukeni kujihusisha na masuala ya kiutendaji hususani suala la kuwa na masilahi binafsi.

“Hapa ni kazi tu”

Kabla ya kuhitimisha hotuba hii napenda kukemea msamiati huu “hewa”.Kama taifa tumepitia wakati mgumu kweli kweli.Kumekuwa na mmomonyoko mkubwa wa maadili kwa watumishi na uzalendo. Ni kama kuna mambo mengi hewa.Hospitali, madaktari hewa, Elimu walimu hewa, wanafunzi hewa, watumishi hewa, miradi hewa, askari hewa!.Mkutano huu unakutanisha wanasiasa watunga na wasimaji sera, vile vile watendaji ambao ni watekeleza sera katika mkoa wa Dodoma ambao ni makao makuu ya nchi. Rai yangu kwenu, fanyeni uamuzi sasa wa kuondoa “hewa” ili kuondoa upotevu wa raslimali za serikali na aibu na kuongeza udhibiti ili hewa zisiwepo tena.

Kwa machache hayo nitamke kuwa Mkutano wa ALAT (M) umefunguliwa rasmi !

Nawatakia kila laheri na kikao chema!

Asanteni kwa kunisikiliza.